# Uhuru na Amani

GAZETI LA KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA TOLEO LA 1, 2015 Bei Sh. 500



## NDANI

Jukwaa la Mazingira laundwa
Mkutano wa Marangu ni nini?
Fahamu sababu za kutofundishwa vipindi vya dini
Hii ni tiba ya moyo ulioshuka
Suluhu yapatikana KKK-Kongo

Vol. 115, Toleo la 1, 2015

ISSN 0856 - 1214

# Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania

## VITABU NA MAANDIKO




Jipatie nakala ya vitabu hivi na maandiko mengine ya Dini toka Dayosisi yako au wasiliana na:

**Idara ya Misioni na Uinjilisti KKKT**

S.L.P. 3033

**ARUSHA**

Barua pepe: elcthq@elct.or.tz

**Uhuru na Amani**
Gazeti la KKKT
**Toleo la 1, 2015**
Vol. 115 Na. 1
**ISSN 0856 - 1214**

Uhuru na Amani ni Gazeti la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT). Hutayarishwa na Kitengo cha Mawasiliano, KKKT.

Maoni yaliyomo katika makala zinazochapishwa ni ya mwandishi anayehusika na wala hayawakilishi mawazo ya Kanisa ama mhariri isipokuwa pale ambapo imetamkwa wazi.

Ukiwa na maoni, ushauri, makala au maswali mwandikie:

**Mhariri**
**Uhuru na Amani**
**S.L.P. 3033**
**ARUSHA**

**Barua pepe:** elobulu@elct.or.tz
**sms** kwa Mhariri: 0754-482-285

**Fungua Tovuti ya KKKT:**
http://www.elct.org/

**MHARIRI**
**Elizabeth Lobulu**

Limepigwa Chapa na:
**Moshi Lutheran Printing Press**
S.l.P 301 Moshi
lutheranpress@yahoo.com

**Newspaper Design & Typesetting:**
**Elizabeth Lobulu**

**Wachangiaji Makala:**
Askofu Ambele Mwaipopo
Mch. Rachel Axwesso
Petrida Batale
Besetina Saikong
Timothy Nyandwale
Faustine Nillan

**picha kwa hisani ya:**
**phillemon fihavango/ kkkt**
**allison westernhoff/ fmkd**
**mchg. anza amen lema/ kkkt**
**mchg. rachel axwesso/ kkkt**
**mchg. luke mwololo/ kelc**

**PICHA YA JALADA:**
Vijana waliohudhuria "Jubilii Kukumbuka Miaka 60 ya Mkutano wa Marangu" toka nchi mbalimbali za Afrika walipanda miti katika Usharika wa Karanga mjini Moshi.
mpiga picha: allison westernhoff

# MAONI YA MHARIRI

**Huu ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu. Tukitazama mfano wa nchi jirani ya Burundi tunajifunza kwamba vita vya wenyewe kwa wenyewe ambavyo siku za nyuma vilisuluhishwa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere na Nelson Mandela wa Afrika ya Kusini vilitokana na masuala ya uchaguzi mkuu.**

**Nchini mwetu uchaguzi unakuja wakati ambapo kuna dalili za uhasama kiasi cha kubaguana kwa itikadi za vyama, ukabila na udini. Tungeomba makundi, asasi mbalimbali na umma kwa jumla tusimamie amani na kila kundi lisiwe kichocheo cha kupalilia uhasama kama inavyoonekana wazi bungeni na kupitia vyombo vya habari nchini, hasa kupitia runinga na redio.**

**Mwaka huu kuna mambo mengi yanayofanywa kwa wakati mmoja kama vile: utoaji wa vitambulisho vya taifa; utoaji wa shahada kwa wapiga kura na lipo wazo la kuwa na Kura ya Maoni kwa Katiba Inayopendekezwa. Utekelezaji wa haya yote sambamba na Uchaguzi Mkuu vinahitaji mipango thabiti na uvumilivu mkubwa kwa wadau wote ili kila jambo liende na kuishia vizuri ilivyokusudiwa.**

**Katika kipindi hichi ni wajibu kwa kila mmoja wetu kufuata sheria, taratibu na maelekezo ya vyombo vya dola. Kwa upande wake vyombo vya dola navyo katika kutimiza wajibu wake kwa ufanisi vinawajibika kutenda haki kwa raia na bila ubaguzi ili kudumisha amani.**

**Kabla ya kura ya maoni au Uchaguzi Mkuu inabidi pawe na vipindi cha kampeni. Ni vema wadau wote wakatumia hekima na kuzingatia makubaliano na taratibu zilizopo ili kampeni hizi zisitumike vibaya na watu wasio na mapenzi mema na taifa letu.**

**Ni jambo jema watu kujitokeza kuingia katika kinyanganyiro cha kutafuta uongozi lakini wapo watu ambao kwa gharama zozote watapenda wapate uongozi. Hivyo kila mmoja wetu awe macho kwa wale wanaotaka kutumia kipindi kama hiki kuwalaghai wenzao kwa lengo la kupata kura.**

**Kwa kuwa kura ni siri ya mpiga kura hata pakiwa na shinikizo kiasi gani, unaweza kushinda endapo kwanza utamwomba Mungu akusaidie kutatafakari na kutambua mtu wa kumpigia kura ili uchague kiongozi anayefaa.**

**Tuendelee kuombea nchi yetu iwe na amani kabla, wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu Tanzania.**

# Rais aaga Kanisa na kutaka watu waombee amani



Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete akimpongeza Askofu Dkt.Stephen Munga wakati wa maadhimisho ya Jubilee ya miaka 125 ya Injili KKKT Dayosisi ya Kaskazini Mashariki yaliyofanyika katika Usharika wa Mbuyukenda, mjini Tanga 5 Julai mwaka huu.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, amewataka viongozi wa dini nchini kuwakemea wanasiasa wanaotaka madaraka kwa kutumia nguvu ya pesa, na kwamba wasiwasikilize wala kuwaendekeza kwani wanataka kulipeleka taifa pabaya na hasa katika kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu.

Rais alisema hayo wakati wa maadhimisho ya Jubilii ya miaka 125 ya Injili ya Dayosisi ya Kaskazini Mashariki ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheli (KKKT) Usharika wa Mbuyukenda, Jijini Tanga.

Alitoa rai kuwa viongozi hao wasiwe sehemu ya wagombea na badala yake watumie nafasi zao kuliombea taifa ili uchaguzi upite kwa uhuru, haki na amani.

Rais pia alizungumzia umuhimu wa kuwa na maadili mema kwa jamii.

Mkuu wa Dayosis ya Kaskazini Mashariki, Askofu Dkt. Stephen Munga, alisema anaamini Rais Kikwete ataivusha nchini salama wakati wa Uchaguzi Mkuu.

## Kanisa lapongezwa kwa amani nchini

Rais Jakaya Kikwete akiwa katika Ibada ya Jubilii ya Miaka 125 ya Injili katika Dayosisi ya Kaskazini Mashariki alisema Serikali ina thamini mchango mkubwa unaotolewa na KKKT katika kujenga umoja, upendo, amani, na mshikamano uliopo baina ya Watanzania wa rangi zote, dini zote, makabila yote na popote watokako na walipo.

## Mbuyukenda kilikuwa kituo cha vijana walikombolewa utumwani

Wamisionari wa Kijerumani wa Chama cha Misioni cha Bethel walianzisha kituo cha kuwahifadhi vijana waliokombolewa toka utumwani eneo la Mbuyukenda, Tanga. Huo ulikuwa mwanzo wa kazi ya kueneza Injili miaka 125 iliyopita na hatimaye kuzaliwa Kanisa la Usambara-Digo.

Pamoja na kueneza Injili ili kumkomboa mwanadamu kiroho, Kanisa pia linaunga mkono jitihada za Serikali kwa kutoa huduma za kijamii.

KKKT Dayosisi ya Kaskazini Mashariki ina Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Sebastian Kolowa (SEKOMU); inamiliki shule za Sekondari Lwandai, Bangala na Dinari; Ina Shule ya Wasioona Irente; Shule ya Msingi ya watoto wenye Ulemavu wa Ubongo (Autism) na ina Kituo cha wagonjwa wa Akili cha Lutindi.

Dayosisi ina hospitali Teule Bumbuli (DDH) yenye Chuo cha Uganga na Hospitali Teule ya Kilindi (CDH).

## Redio Utume kuanza karibuni

Dayosisi ya Kaskazini Mashariki yenye makao yake Lushoto, Tanga imeanzisha Kituo cha Redio Utume ambacho kinatarajiwa kuanza kurusha matangazo yake hivi karibuni baada ya kupatikana leseni ya utangazaji kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

# Hospitali zapata vyombo vya usafiri

Katibu Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Bw. Brighton Killewa, 16 Juni mwaka huu alikabidhi vyombo vya usafiri kwa ajili ya Huduma ya Tiba Shufaa katika Hospitali mbili za Dayosisi za KKKT. Hospital hizo ni Hospitali Teule ya Ilula CDH inayomilikiwa na Dayosisi ya Iringa iliyopewa gari na Hospitali Teule ya Kilindi CDH inayomilikiwa na Dayosisi ya Kaskazini Mashariki iliyopokea pikipiki. Vyombo hivyo vya usafiri vimepatikana kwa uhisani wa Kanisa la Kilutheri la Marekani na Shirika la Misaada la Marekani. Hafala hiyo fupi iliyofanyika Ofisi Kuu ya KKKT, Arusha ilihudhuriwa na viongozi na watumishi wengine. Kitengo cha Huduma ya Tiba Shufaa KKKT kina watumishi wawili: Mratibu Dkt. Zebadia Mmbando na Sista Anna Mahenge.



Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa, akikabidhi ufunguo wa gari kwa Katibu Mkuu wa KKKT Dayosisi ya Iringa, Bw. Naiman Chavalla (kulia), huku Mganga wa Hospitali ya Ilula, Dkt. Erasto Rite akishuhudia.



Katibu Mkuu wa KKKT (katikati) na NKM Misioni na Uinjilisti KKKT, Mch. Lazaro Rohho, wakishuhudia Mratibu wa Huduma ya Tiba Shufaa Hospitali ya Kilindi, Bw. Isaya Kilindo, akiwasha pikipiki ambayo ilikabidhiwa kwa Muuguzi Mfawidhi wa Hospitali ya Kilindi, Bw. Cosmas Mwacha (hayupo pichani).

# KKKT yaanzisha Kituo cha Utamaduni

Mkuu wa KKKT ambaye pia ni Mkuu wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira (TUMA), Askofu Dkt. Alex Malasusa, 15 Mei mwaka huu aliweka jiwe la msingi na kuzindua Kituo cha Utafiti, Utamaduni na Sanaa Chuoni Makumira. Lengo lake ni kuhifadhi na kuinua kazi za utamaduni na sanaa katika Ukanda wa Kaskazini mwa Tanzania. Kituo hicho cha utafiti kimepata uhisani wa Umoja wa Ulaya. Wasiliana na Bw. Randy Stubbs +255786300213 tovuti: www.cac.makumira.ac.tz




**Askofu Malasusa, Bi Alexa du Plessis, Mwakilishi wa Balozi wa Umoja wa Ulaya (EU) na Meneja wa Programu hiyo Bw. Randy Stubbs ambaye pia ni Mratibu Kitengo cha Muziki TUMA.** picha kwa hisani ya r. stubbs

## KKKT Yatoa Takwimu Mpya ya Idadi ya Washarika Wake

Takwimu zilizotolewa hivi karibuni na Uongozi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) zinaonesha Washarika wa Kanisa la KKKT walifika 6,531,336 mwaka 2014.

Mwaka 2013 KKKT ilikuwa na Washarika 6,341,103.

Kwa maelezo zaidi kwa miaka ya nyuma fungua tovuti ya KKKT: www.elct.or.tz au www.elct.org.

## Mameo ashinda kura ya imani

Mkutano Mkuu wa Dayosisi ya Morogoro uliofanyika Mwezi Juni ulimpigia Askofu Jacob Ole Paulo Mameo kura ya imani na kumtaka aendelee kuongoza dayosisi hiyo.



**Askofu Jacob Ole Paulo Mameo, KKKT Dayosisi ya Morogoro.**

## Massangwa ahimiza ujirani mwema



**Askofu Solomon Massangwa, KKKT Dayosisi ya Kaskazini Kati.**

Askofu Solomon Massangwa wa Dayosisi ya Kaskazini Kati amesisitiza mshikamano kati ya wananchi wanaoishi mipakani mwa nchi kwa kuwa asili yao ni moja.

Askofu Massangwa alisema hayo hivi karibuni katika Ibada na mazungumzo ya ujirani mwema ambayo hufanyika kila mara kuwakutanisha viongozi wa Kanisa la Kilutheri wanaofanya kazi ya Injili katika mpaka wa Tanzania na watumishi wenzao kutoka Kenya.

# Askofu Mpya Kaskazini Magharibi



**Mchg. Dkt. Abednego N. Keshomshahara, Askofu Mteule Dayosisi ya Kaskazini Magharibi.**

*Na Petrida Batale*

Mkutano Mkuu wa Dayosisi ya Kaskazini Magharibi hivi karibuni ulimchagua Mchg. Dkt. Abednego Nkamuhabwa Keshomshahara kuwa Mkuu wa Dayosisi hiyo kuchukua nafasi ya Askofu Elisa Buberwa anayetarajia kustaafu Oktoba mwaka huu.

Mchg. Keshomshahara alizaliwa 2 Februari 1969 Kijiji cha Ngando, Wilaya ya Misenyi, Kagera. Alibarikiwa kuwa Mchungaji 14 Desemba 1997. Ana Shahada ya Udaktari wa Falsafa (PhD) katika Theolojia. Kwa sasa ni Mkufunzi Chuo Kikuu Kishiriki cha Josiah Kibira (JOKUCO) na Msaidizi wa Mkuu wa Chuo (Utawala). Mchg. Keshomshahara ameoana na Melisa na wamebarikiwa watoto wawili.

Mkutano huo mkuu uliofanyika Shule ya Msingi Kibeta mjini Bukoba 2 Juni 2015 ulifunguliwa na Mkuu wa KKKT Askofu Dkt. Alex Malasusa. Neno Kuu lilitoka Kitabu cha Waamuzi. 4: 8a, 9a.

## Kongamano la Vijana laandaliwa

Kongamano la Nne la Vijana wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) litakalo hudhuriwa na vijana wapatao 1,000 linatarajiwa kufanyika mwaka huu mjini Dodoma.

Mratibu wa Vijana KKKT, Mchg. Anza Amen Lema, alisema hivi karibuni kwamba washiriki ni vijana toka Dayosisi za KKKT na Maeneo ya Misioni.

Mwaka 2013 Kongamano la Vijana lilifanyika Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, Arusha.

# SOMO LA BIBLIA

# “Angalia, ukatulie, usiogope na usife moyo,” (Isaya 7: 4)

## UTULIE

Maneno haya: ***“Angalia, ukatulie, usiogope na usife moyo,”*** (Isa 7: 4) yanatia matumaini mioyo inayotaka kuzimia. Ukiwa una panda mlima mrefu na kukutana na mtu anayeshuka akakuambia ‘***kileleni si mbali, ninatoka huko na wewe unakaribia kufika.’*** Hakika hata kama umechoka sana nguvu itazaliwa, ari ya kuendelea itakujia na utaendelea na safari hadi mwisho. Maneno ya kutiwa moyo yakikosekana ni hasara kwani maono, fursa na ndoto zitaharibika.

***Mungu si mwanadamu*** bali ni wa huruma ***anayetupa nafasi ya kujirekebisha kila wakati.*** Ayubu alipopita mapito magumu ***alivaa matumaini ambayo yalilisha imani yake*** (Ayu 1: 21) **Pia soma** Ayu 14: 7 - 9.

Mfuate Mungu na tulia naye, ***usiogope na usife moyo***. Hata daktari akisema ‘sasa basi,’ ***Mungu anaweza*** licha ya kuwepo mvutano kati ya Mungu na Shetani kwa sababu kuna kitu kikubwa cha thamani kilicho ndani yako na kipimo ni imani uliyonayo. Hata Bwana wetu Yesu Kristo alipambana na mateso kwa vile Yeye ndiye **“*thamani ya wokovu wetu.*”**

Mungu hutuandalia msingi imara wa kupokea baraka lakini kuna watu baraka zao zimepitishwa kwa walezi wao kwa sababu ya ‘utoto wao kiroho’. Mti wa matunda hupigwa sana kwa mawe na mwamba wenye madini umechorongwa sana. Maana yake ni kwamba mapigo au changamoto zako zinatokana na thamani iliyo ndani yako. Mateso ya watu wa imani kama Ayubu, Ibrahimu, nk., ni mengi sana. Na Biblia iko bayana: “***Hatuitwi tu ila ni pamoja na mateso.” Angalia, tulia, usiogope na usife moyo.*** Changamoto ni je nitajihakikishiaje ushindi? Washindi wana alama katika moyo. Na katika hizo alama Mungu anatengeneza fursa, hali, mazingira, maisha mapya, ndoto, mipango na maono mapya. Yesu aliyetuweka kwa kusudi hilo atatushindia. Ogopa sana kuitwa na wanadamu utaanguka vibaya. Lakini ***katika Kristo tuna nguvu na ujasiri wote*** (Efe 5:4). ***Yesu ni jiwe kuu la pembeni*** wote waliaminio watapata faida na baraka za roho na mwili pia.

***“Mauti ilimezwa kwa kushinda kwake,”*** (1Kor 15: 54). Ilipomezwa, kaburi halikuweza kumzuia Yesu asitoke kaburini. Nasi tumevikwa uzima (Zab 82: 6). Tuliookoka na kuvaa Roho ya Kristo, nguvu za giza, pepo yote, roho chafu ya ulimwengu wa giza zijue sisi tumevaa mamlaka hayo. ***Vaeni silaha za rohoni*** (Efe 6: 11) Hakuna nguvu iliyo juu kuliko yake.

## USIFE MOYO

Ugonjwa wa kufa moyo ni mbaya sana. ***Moyo wako ... ndiko zitokako chemchemi za uzima*** (Mit 4: 23). Moyo wenye uchungu ni rahisi kuingiliwa na adui kwa njia mbalimbali hata magonjwa. Moyo



**Mchg. Rachel Axwesso**
**Naibu Katibu Mkuu Huduma za Jamii na Wanawake, KKKT**

dhaifu ni maisha dhaifu. Usiruhusu moyo wako uwe kama jalala la takataka. Moyo dhaifu unazuia baraka. Ondoa uchungu. Mungu anatamani sana kukubariki. Moyo uliochangamka ni dawa nzuri ya maumivu moyoni. ***Angalia, tulia, usiogope na usife moyo***. ***“Mungu ni mwamba wa moyo wangu na sehemu yangu,”*** (Zab 73: 26). Hivyo usiangalie shida yako na kudhani ni kubwa kuliko uwezo wa Mungu. Hata ukichoka usivae huzuni usoni mwako. ***Mbona umesikitika na uso wako?*** (Neh 2: 5). Shetani huangalia uso wako na kutafuta jinsi ya kukukatisha tamaa.

Raheli alikataa kufarijiwa alipowalilia watoto wake walipopelekwa utumwani (Yer 31: 15). Nafananisha tatizo lake na la wasichana wa Nigeria wanaotekwa na Boko Haram. Wanawake waliowazaa uchungu wao ni mkubwa sana. Jibu la Mungu ni kwamba: ***Zuia sauti yako usilie macho yako yasitoke machozi maana kazi yako itapata thawabu*** (Yer 31: 16). Soma **Kut 14: 13 - 14.**

Tunapojaribiwa Mungu anabeba mambo yote yaliyo juu ya uwezo wetu. Jina la Mungu **‘Jehova Shamali’** maana yake ni ‘Mungu mwaminifu’. Mwite ataitika. Shedraka, Meshaki na Abednego kwenye hatari ya kuangamizwa kwa moto waliona nguvu za Mungu. **Jehova Shamali** alishuka na kuwaokoa (Dan 3: 25). Usiogope Jehova akishuka mambo makubwa yanatokea. Mfano barabara iliyotokea baharini (Kut 14: 17 -21) na majeshi ya Wamisri kuangamizwa (Kut 14: 28). Ondoa hofu Mungu akiwa kazini hakuna anayeweza kufungua, kupinga au kuzuia alilokusudia kwamba ni kazi ya mikono yake, (Yn 14: 13 -14). Thubutu kwa imani. Yeye Mungu atakufanyia yote kwa upendeleo wa hali ya juu.

**Jehova Shamali** alipogusa matumbo tasa, yalipokea baraka ya watoto. Na hata milango iliyofungwa itafunguka. Usiogope, subiri, vumilia hajakusahau. Soma Isa 43: 1.

***Jehova Nissi*** maana yake: Bwana ni bendera yangu (Kut 17: 15 - 16). Yehova Nissi ni Mungu mpiganaji katika vita vyote (Zab 46: 1-3). Amka maana Shetani ameshindwa. ***Adui ajapotokea kwa njia moja atakimbia kwa njia saba. Jehova Nissi*** hasinzii, hachoki, akili zake hazichunguziki (Isa 40: 28). ***Jehova Nissi*** anatutia moyo na ujasiri (Kut 23: 27). ***Jehova Nissi*** akishuka vita na mateso hayatainuka tena (Neh 1: 9). Pia soma **Isa 41: 10.** Mikono ya madaktari ikishindwa kamwe mikono ya Yesu / Mungu haitashindwa.

Endapo milango imefungwa na haitafunguka tena. Wala usibaki kulia mbele ya mlango uliofungwa. Unateseka unadhoofika na unachoka na mwisho wa yote ni uharibifu ndani ya huo mlango. Chunguza uone mlango wako mpya wa faida. Mungu haanzi kufunga mlango bali anafungua kwanza mlango wa faida ndipo anafunga mlango wa hasara. Katika mlango huo mpya Mungu anataka kufanya au kutenda mambo makubwa na ya faida kwako. Usililie mlango wa hasara uliofungwa na Mungu maana mambo/ baraka zako haziko humo. Mungu amehamishia baraka zako kwenye mlango mwingine. Tazama na kusikiliza kwa makini. Yakobo aliambiwa na Mungu aondoke kwa Laban ***“Sasa uondoke toka katika nchi hii urudi mpaka nchi ile uliyozaliwa,”*** (Mwa 31: 13b). Maana yake ni kwamba mlango wa kukaa kwa Laban ulikwishafungwa.

***Jehova Yire*** maana yake ***‘katika mlima wa Bwana anapatikana’*** (Mwa 22: 14). Baada ya jaribu la kutaka Ibrahimu amtoe sadaka Isaka, Mungu alitoa kondoo badala ya Isaka na ndipo Ibrahim alijenga madhabahu na kuiita ***Jehova Yire. Yehova Yire*** ni Mungu anayeachilia mahitaji yetu yote tumwombapo. Soma pia Mt 6: 31 – 32. Jehova anajua tunachokihitaji. Maombi yako ni mshale unaopenya hadi kwenye chumba cha kiti cha enzi cha Mungu na kurudi na baraka zako. Mungu akishuka mabadiliko yanatokea: hata magonjwa yanapona; uchumi unaimarika; mateso, dhiki, taabu zinakoma; ukandamizi unakoma na unyonge unabadilika kuwa nguvu. Usiogope kumngoja Bwana. Ni hakika kwamba ***Jehova Yire*** atawavika nguvu, uweza, nk. (Yer 23: 23).

***Jehova Shalom*** maana yake ni ***‘Mungu wa amani.’*** Ni Mungu mwaminifu sana. Wakati wa mitikisiko, hari, kimbunga, mawimbi watu walisali, dhoruba ikakoma. ***Jehova Shalom*** ni mjenzi wa amani. Mkaribishe Yeye Shalom - ahusike na amani yako. ***“Wanafunzi walifunga milango kwa hofu ya Wayahudi”*** (Yn 20: 19). Amani iwe kwenu (Yn 20). Yesu ndiye amani. Mtafute upate amani yako. Linda imani yako kwa maana inabeba baraka zako

*endelea uk. 7*

## Kanuni za kutazama ni zipi?

*inatoka uk. 6*

(msaada wako). Ushindi huja kwa jina la Yesu/ Mungu. Somo hili kuhusu **Isa 7: 4** linaanza na maneno***"angalia"*** au tazama.

**Kanuni za Kutazama**

Ziko baraka za kutazama. Kanuni ya kwanza katika kutazama ni kwamba inatupasa **'tuwe makini'** ili kuona fursa zilizopo mbele. Jangwani wana wa Israeli "walitazama" nyoka ya shaba ikawa uponyaji kwao (Yn 3: 14).

Kanuni ya pili ni **kutulia**. Tulia usikilize sauti ya Mungu. Askari vitani husikiliza sauti ya aliye juu yake. Aaminiye hatafanya pupa katika mambo yake. **Soma Lk 9: 54 - 55. *Usiogope na usife moyo.*** Pia Soma **Yer 16: 21, Isa 43: 1.**

Kanuni ya tatu ni **kungoja**. Kipindi cha ***kumngoja Mungu kwa matumaini hadi kupokea,*** kinawachanganya watu wengi. Kinahitaji moyo wa uvumilivu na neema ya Mungu. Kushindwa kungoja ni kupoteza, na hivyo kukosa. Kusubiri ni gharama lakini yenye faida. Mashujaa wa imani Ibrahimu (miaka 100) na Sara (miaka 90) walingoja mrithi. Daudi alingoja kipindi cha kutawadhwa. Nuhu alingoja mvua kwa miaka 120. Kanuni nyingine ni **maombi**. Tuwe kama Hana shujaa wa maombi. Alisubiri muujiza wake (Isa 1: 14 - 15). Hatimaye alipokea mtoto mwanamume alivyoomba. Hata wewe Mungu atakupa utakachomwomba.

**HITIMISHO**

Uvumilivu ni kusimama imara, kubaki mwenye nguvu na kuendelea na safari uliyoianza hata ikiwa na upinzani, ugumu, vikwazo na majaribu. Ni uwezo wa kuendelea na yote bila kukata tamaa hata upatapo hasara katika biashara, nk.

Ili kupokea uombacho yafuatayo ni muhimu: Usikate tamaa, baki na ujasiri wala usibadili nia ya kwanza kwa mfano kwa kupokea maoni mengine. Tawala akili zako maana adui hayuko mbali yuko moyoni mwako. ***Vumilia mpaka mwisho*** (Mt 24: 18). Tembea na Mungu mpaka mwisho. Baki uki***angalia, tulia, usiogope.*** Pia soma **Yer 16: 21.**


Huuwezi kukwepa uwepo wa Mungu hapa duniani. Tena hauwezi kuacha kumpa Mungu mashauri yetu. Yeye ni mwema. ***'Nitafanya agano la milele pamoja nao, kwamba sitageuka wala kuwaacha, ili niwatendee mema; nitatia kicho changu mioyoni mwao, ili wasiniache,' (***Yer 32: 40***).*** Mwite Mungu ni mkuu. Kwa mambo yote Mungu ni mweza. ***Niite, nami nitakuitika, nami nitakuonyesha mambo makubwa, magumu usiyoyajua*** (Yer 33:3).

Daudi aliyemuua Goliathi alisema: ***"Mimi ninakujia wewe kwa jina la Bwana wa majeshi, Mungu wa majeshi ya Israeli uliowatukana,"*** (1Sam 17: 45). Ndipo Goliath wa Gathi aliuawa kwa kombeo. Silaha za upanga, mkuki na mvumo hazikufaa kitu. Vita vya Bwana havihitaji nguvu zetu bali imani zetu.

Linda imani yako usije ukapata hofu, wasi wasi, mashaka na kukata tamaa. Usiangalie nyuma kutazama unyonge uliopita. Yajayo hayajengwi kwa mambo yaliyo pita na hasa yakiwa madhaifu. **Amen.**

**Mchg. Rachel Axwesso** ni mwandishi wa vitabu.
Anapatikana kwa e-mail: <rahelijo@yahoo.com>

# Fungamano lakumbuka Jubilii ya 60 ya Mkutano wa Marangu



**Bw. Brighton Killewa, Katibu Mkuu wa KKKT.**

Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD) liliandaa Kongamano lililowakutanisha takriban watu 200 kutoka sehemu mbalimbali duniani kukumbuka Mkutano wa Kwanza wa Viongozi Makanisa ya Kilutheri Afrika (Africa Lutheran Church Leaders Conference), uliofanyika katika Chuo cha Ualimu Marangu, Mkoani Kilimanjaro mwaka 1955.

Katibu Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Bw. Brighton Killewa, ameeleza kwamba Kongamano lilifanyika Uhuru Hotel Moshi 20 - 24 Mei 2015. Ibada rasmi ya kilele cha Jubilii ilifanyika Marangu Mei 24.

Lengo la Jubilii hiyo lilikuwa ni kuenzi ***Urithi Wetu*** uliotokana na ***Matengenezo ya Kanisa na kuhuisha roho ya umoja miongoni mwa Makanisa ya Kilutheri Afrika*** iliyoanzishwa katika ***Mkutano wa Marangu*** 1955.

Kongamano hilo liliongozwa na Neno toka ***Warumi 12: 1 - 5*** chini ya kauli mbiu: ***"Kutoka Marangu kuelekea Wittenberg."*** Majadiliano yalielekezwa katika "Mafunzo ya Theolojia" na "Uongozi na Matengenezo ya Kanisa la Kilutheri Barani Afrika."

Viongozi wa Makanisa ya Kilutheri Barani Afrika walitumia fursa ya Kongamano kuweka mkakati wa safari kuendea maadhimisho ya jubilii ya ***Miaka 500 ya Matengenezo ya Kanisa*** ambapo kilele chake kitakuwa jijini Wittenburg, Ujerumani 2017.

Kongamano hilo lilikuwa na matukio kama: Warsha ambapo washiriki kutafakari "tulikotoka na tunakoelekea katika safari ya ***Matengenezo ya Kanisa."*** Mengine yaliyofanyika ni mikutano ya uongozi wa FMKD; mikutano ya viongozi (Africa Lutheran Church Leaders Conference), mikutano ya wawakilishi wa wanawake na wa vijana. Baadhi yawajumbe walifanya ziara maeneo mbalimbali.

Mada zilizojadiliwa ni: ***Wokovu usiuzwe*** (Mdo 8: 18 - 20); ***Uumbaji ni wa kutunzwa sio bidhaa ya kuuzwa*** (Mwanzo 2: 15); ***Binadamu maskini wasiuzwe utumwani*** (Amosi 8: 6); Yakobo 5: 1 - 4) na ***Tumekombolewa kwa Neema ya Mungu*** (Yn 10: 10).



**Maandamano kabla ya kuanza Ibada ya kufunga Kongamano la Jubili ya Mkutano wa Marangu.**

# Umoja na mshikamano umeimarisha Kanisa Afrika

**Na Elizabeth Lobulu**

Makamu wa Rais wa Fungamano la Makanisa Duniani (FMKD) Kanda ya Afrika, Askofu Dkt. Alex Malasusa ambaye pia ni Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), alisema hivi karibuni kwamba Kanisa la Kilutheri barani Afrika limekua na kuimarika kutokana na roho ya umoja na mshikamano iliyopandikizwa na viongozi wa Kanisa walipokutana kwa mara ya kwanza Chuo cha Ualimu Marangu, mkoani Kilimanjaro mwaka1955.

Mkutano huo wa Marangu ulikuwa chimbuko la kuanzishwa kwa Jumuiya ya Makanisa ya Kilutheri Barani Afrika.

Akifungua Kongamano 22 Mei mwaka huu mjini Moshi, lililohudhuriwa na washiriki 200 kuadhimisha miaka 60 tangu Mkutano wa Marangu ufanyike, aliwaasa viongozi na washarika waimarishe umoja ili lengo la Kanisa la kumhudumia mwanadamu kimwili, kiakili na kiroho barani Afrika litimie.

# Afrika tumieni nguvu ya umoja kutatua migogogro- Junge



Wajumbe na wageni waalikwa baada ya Ibada ya ufunguzi Kongamano la Jubilii ya Miaka 60 ya Mkutano wa Viongozi wa Kilutheri Afrika uliofanyika Marangu.

Katibu Mkuu wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD), Mchg. Martin Junge, alihimiza makanisa ya Kilutheri Afrika kutumia vema mshikamano wao ili kutetea haki, amani na kuleta suluhu ya migogoro Afrika.

Akizungumza katika Kongamano lililoandaliwa na FMKD kukumbuka miaka 60 ya Mkutano wa Marangu, alipongeza makanisa yaliyokuwa mstari wa mbele kwa uthubutu na uamuzi wa kuja pamoja barani Afrika licha ya kukabiliwa na mzigo mzito, kwa kuwa bado yalikuwa chini ya ukoloni.

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) lilikuwa mwenyeji wa Kongomano hilo lililonyika 20 - 24 Mei 2015.

Mchg. Junge pia alielezea kuhusu jubilii ya miaka 500 ***Matengenezo ya Kanisa*** na Mkutano Mkuu wa 12 wa FMKD utakaofanyika 2017.

Kongamano lilikuwa na warsha na mikutano kwa makundi mbalimbali ukiwemo



**Mchg. Martin Junge**
**Katibu Mkuu FMKD**.

Mkutano wa Viongozi wa Makanisa ya Kilutheri Afrika ***(The Africa Lutheran Church Leadership Conference).*** Viongozi hao walijadili kwa kina ***Matengenezo ya Kanisa katika mtazamo wa Afrika inayobadilika.*** Mada kadhaa zilijadiliwa kuhimiza kazi ya kanisa la leo kuhakikisha kwamba **'uumbaji sio bidhaa ya kuuzwa', 'wokovu usiuzwe'** na **'binadamu waheshimiwe na wasiuzwe kama bidhaa'.**

Mchg. Junge aliwakumbusha wajumbe msimamo na FMKD unaosisitiza umoja na utambulisho wa Walutheri na kusema kwamba wokovu unapatikana kwa imani tu na siyo kutokana na hadhi tuliyonayo na kazi au ngazi tulizonazo bali ***ni kutokana na Mungu wetu alivyo na yale ayatendayo.***

Kongamano liliratibiwa na Dawati la Kanda ya Afrika katika Idara ya Misioni na Maendeleo ya FMKD.

Katibu wa Dawati la Afrika FMKD, Mchg. Dkt. Elieshi Mungure, alisema Kongamano lilisisitiza umuhimu wa kutatua matatizo ya kijamii na kiuchumi barani Afrika kama rushwa na mabadiliko ya tabianchi. Pia wajumbe walijadili umuhimu wa kuandaa mipango endelevu katika Kanisa.



**Mchg. Dkt. Elieshi Mungure.**
**Katibu Dawati la Afrika, Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani.**

# Tunzeni uumbaji wa Mungu - vijana

Vijana wawili toka wa KKKT Bw. Harold Minja (26) na Bw. Dawson Chonjo (32) walipandisha bango juu ya Mlima Kilimanjaro (mita 5,892.8) ili kuhamashisha jamii kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira (uumbaji). Vijana hao waliwakilisha washiriki 200 waliokuwa Tanzania kushiriki Kongamano la Jubilii ya Miaka 60 ya Mkutano wa Marangu. Walikabidhi bango hilo wakati wa Ibada iliyofanyika Chuo cha Walimu Marangu 24 Mei. Watu wapatao 2,000 walihudhuria Ibada hiyo. Kilimanjaro ni mlima mrefu kuliko yote Afrika.

# TOLEO MAALUMU

# Fahamu Huduma ya Kitengo cha Utetezi KKKT

## UMUHIMU WAKE

Umuhimu wa kuwa na ***Kitengo cha Utetezi*** kwa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) ulijitokeza wazi mwaka 1994.

Maaskofu wa KKKT walikutana 9 - 13 Machi 1994 kujadili mustakabali wa taifa katika haki za kiuchumi na maendeleo. Pamoja na mambo mengine Maaskofu walitoa ***"Tamko la Bagamoyo"*** na kupendekeza Kitengo kianzishwe.

Baada ya maandalizi ndipo Kitengo cha Utetezi cha KKKT kilianzishwa 1999 wakati huo kilijulikana kwa jina ***Dawati la Haki za Binadamu na Utetezi.***

Mwaka 2000-2010 kitengo kilishirikiana na viongozi wa dini na madhehebu mengine kufanya makongamano na kutoa matamko yaliyoandikwa kama vijitabu vidogo vidogo kuhusu biashara ya haki kimataifa (fair trade) kwa mazao kama chai, pamba na kahawa; tatizo la rushwa katika uchaguzi, nk. Pia walitoa ***Tamko la Dar es Salaam*** kuhusu Uchumi.

***Mwongozo wa Elimu ya Uraia*** ulitolewa kwa ajili ya Dayosisi zote za KKKT na semina kuhusu elimu ya uraia kipindi kinachokaribia uchaguzi mkuu ziliendeshwa katika ngazi ya Serikali za Mitaa na Kitaifa ili kuwakumbusha raia wajibu na haki zao.

Kwa sasa ***Kitengo cha Utetezi*** kinapata ufadhili wa ***Danmission*** (Denmark) pamoja na ofisi ya ***Norwegian Church Aid (NCA)*** iliyopo Dar es Salaam.


**Wasiliana na Mratibu**

**Dawati la Utetezi KKKT**

<besetinas@gmail.com>


# Mradi wa kuondoa Ukatili ulivyoanza



***Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Alex Malasusa, baada ya kuongoza Ibada ya Uzinduzi wa "Mwongozo wa Masomo ya Kuondoa Ukatili katika Jamii."***

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania na Danmission wameshirikiana katika ***Mradi wa Kuondoa Ukatili katika Jamii*** tangu mwaka 2011.

Mradi ulianza kwa kuandaa ***Mwongozo wa kufundisha masomo ya kuondoa ukatili katika jamii (Training Manual to Combat Community Violence)*** na baadaye ulihusika kutoa elimu katika maeneo husika.

Mradi huu ulikuwa wa majaribio kwa miaka mitatu, 2011-2013 kwa Dayosisi tatu za Ukanda wa Ziwa ambazo ni: Dayosisi Masharikiki ya Ziwa Vicktoria, Dayosisi ya Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria na Dayosisi Mkoani Mara.

Tathmini ya mradi ilifanyika na ilionesha mafanikio makubwa sana. Mapendekezo yaliyotolewa na walengwa wa mradi yalikuwa chanya na hivyo, mradi ukapewa awamu nyingine ya utekelezaji.



**Askofu Michael Adam, KKKT Dayosisi Mkoani Mara (kushoto) akifuatiwa na Askofu Andrew Gulle, KKKT Dayosisi Mashariki ya Ziwa Vicktoria (DMZV) na Askofu Emmanuel Makala, KKKT Dayosisi Kusini Mashariki ya Ziwa Vicktoria Aprili 2014 walishiriki mkutano uliohudhuriwa na Waratibu wa Dawati la Utetezi wa Dayosisi tano za Ukanda wa Ziwa na wa kutoka Ofisi Kuu ya KKKT.**

**Viongozi hao walipokea ripoti ya maendeleo ya kazi za mradi katika dayosisi hizo; walijadili changamoto na kushiriki kutoa maoni kuhusu mbinu mbadala za kuondokana na ukatili katika jamii katika maeneo yao. Mwanamke mmoja aliyeshiriki alikubali kuacha kazi ya ungariba baada ya kutambua madhara ya ukeketaji wanawake ila akaomba viongozi hao wa Kanisa wamsaidie njia mbadala ya kumpa kipato.**

Wakati huo huo Mkutano Mkuu wa KKKT Dayosisi Mkoani Mara na Mkutano Mkuu wa KKKT Dayosisi Mashariki ya Ziwa Victoria iliyofanyika mwaka jana imewapa ridhaa maaskofu wao kuendelea kuongoza.

# Utetezi wa Sera Katika Ngazi ya Taifa

Ofisi ya Shirika la Misaada Kanisa la Norway (***Norwegian Church Aid)*** iliyopo Dar es Salaam inahisani ***Mradi wa Utetezi wa Sera KKKT***. Kazi kubwa ni kufanya ***Utetezi wa Sera*** katika ngazi ya taifa. Utetezi unafanywa baada ya Sera zilizobainishwa kufanyiwa uchambuzi na mapendekezo stahiki kutolewa. Ifikapo hatua hiyo ndipo ***Kitengo cha Utetezi KKKT*** kinashirikisha ***Kamisheni ya Haki na Amani KKKT*** na Viongozi wa kiimani (CCT, TEC, BAKWATA na PCT) ili kuwa na uelewa wa pamoja wa changamoto zilizopo na kutoa mapendekezo yao. Kitengo kinajukumu la kuwakutanisha viongozi wa dini na Viongozi wa Wizara au Kamati husika za Bunge.





Askofu Dkt. Stephen Munga Mwenyekiti wa Kamisheni ya Haki na Amani KKKT akiongea na Wabunge mjini Dodoma.




Wabunge wakisoma mojawapo ya mabango yaliyoandaliwa na KKKT.



Mratibu wa Kitengo cha Utetezi KKKT, Bibi Besetina Saikong akifuatilia mdahalo wa viongozi wa dini wa Mikoa ya Arusha na Manyara walipojadili namna ya kukabili mabadiliko ya tabianchi.
Wasiliana naye kwa barua pepe: <besetinas@gmail.com>

## Lengo ni kuboresha sera

Lengo kubwa la Mradi wa ***Utetezi wa Sera Kitaifa*** ni kutoa mapendekezo na kufanya ushawishi kuhusu sera husika ili zirejewe na ziweze kubadilishwa inavyostahili. Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania na NCA wameshirikiana katika masuala ya: ***Mabadiliko ya Tabianchi,*** kwa kuwawezesha viongozi wa dini kuwa na mazungumzo ya pamoja na watendaji katika Wizara za Maliasili na Mazingira, Wizara ya Nishati na Madini na Kamati za Bunge zinazohusu Mazingira.

Aidha, ***Kitengo cha Utetezi*** KKKT pamoja na ***Kamisheni ya Haki na Amani*** KKKT wameendelea kukutana na viongozi wa Serikali ili kufuatilia kwa karibu marejeo ya sera zenye kuhitaji mabadiliko kwa manufaa ya wananchi kwa maendeleo chanya ya Taifa letu.

Kitengo cha Utetezi kuanzia 2014 kimeanza kuchambua ***Sera ya Taifa ya Jinsia Wanawake na Watoto*** ili kuona mambo ya kuboreshwa. Pia Kitengo kinapitia sheria zinazochangia ***ukatili wa kijinsia.*** Zipo sheria nane (8) zilizobainishwa na ufafanuzi utatolewa kuhusu adhari zake kijamii na kitengo kinatafuta maoni ya dini ya Kikristo na Kiislamu kuhusu sheria hizo.

# MDAHALO: MABADILIKO YA TABIANCHI



Bw. Nyerembe Mnasa, aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Arumeru.




Bw. Brighton Killewa, Katibu Mkuu wa KKKT akieleza lengo la mdahalo.

***Kitengo cha Utetezi*** cha Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), kiliandaa mdahalo wa wadau wa mazingira kutoka Wilaya za Mikoa ya Arusha na Manyara 15 Oktoba 2014.

Akifungua mdahalo huo, Mkuu wa Wilaya ya Arumeru kwa wakati huo, Bw. Nyerembe Mnasa, alikumbusha viongozi wote wa kijamii kuwajibika katika nafasi zao ili kutunza mazingira na kuondoa mambo yanayosababisha ***mabadiliko ya tabianchi.*** Pia alilipongeza Kanisa kwa kuandaa mdahalo huo muhimu.

Viongozi wa dini/ madhehebu; watendaji Sekta ya Mazingira wa Halmashauri za Wilaya; Madiwani, wawakilishi wa Asasi za Kiraia; watafiti; maafisa waandamizi toka Idara za Mazingira na Maliasili, Kilimo na Mipango Mkoa wa Arusha na waandishi wa habari walihudhuria.

Akimkaribisha Mgeni rasmi, Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa, alieleza lengo la mdahalo huo ni kushirikiana ili hatimaye kuanzisha majukwaa ya kuelimisha jamii kuhusu ***mabadiliko ya tabianchi na uhifadhi wa mazingira*** kuanzia ngazi za vitongoji/ mitaa/ vijiji na Kata.

## Mapendekezo ya washiriki wa mdahalo

Tatizo la ***mabadiliko ya tabianchi*** chanzo chake ni kuongezeka kwa ***hewa ukaa*** duniani. Hivyo washiriki wa mdahalo walipendekeza taasisi za kiimani, asasi na wadau wa mazingira waelimishe watu wote kuanzia ngazi ya kaya hadi taifa juu ya athari za: ***Ukataji miti ovyo na ufekaji misitu; Kutokuwa na mipango mizuri ya uhifadhi/ matumizi ya ardhi na kutodhibiti sumu na taka za viwandani /migodini.*** Mengine ni athari za: ***Uwindaji haramu wa wanyama pori; Kutotunza vyanzo vya maji na kuto hifadhi ardhi maeneo ya migodi, fukwe za mito/ bahari na kutozingatia kilimo, ufugaji na uvuvi bora.***

Washiriki walitoa wito kwamba watu katika kila ngazi watekeleze mipango / miradi mbadala ili kuzuia uharibifu wa mazingira na kupunguza kasi ya ***mabadiliko ya tabianchi.*** Kila mtu ana wajibu wa ***kutunza uumbaji wa Mungu.***

Pamoja na mambo mengine, wajumbe walipendekeza kamati ndogo ya kupanga jinsi ya kuunda "***Jukwaa la Mazingira na Tabianchi"*** katika mikoa ya Arusha na Manyara.



Washiriki wa Mdahalo kuhusu uhifadhi wa mazingira na jinsi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika Wilaya za Mkoa wa Arusha na Manyara.

# Jukwa kukabili mabadiliko ya tabianchi kuundwa



Washiriki wa mdahalo uliohudhuriwa na watu 62 toka Wilaya za Mikoa ya Arusha na Manyara walipendekeza liundwe ***Jukwaa la Mazingira na Tabianchi kwa Wilaya za Mikoa ya Manyara na Arusha.*** Kamati ndogo kutoka dini na madhehebu mbali- mbali iliundwa ili kutoa mapendekezo ya kuanzisha jukwaa.

Waliochaguliwa ni Sheikh Abdallah Masoud, ***Katibu wa BAKWATA Mkoa wa Arusha;*** Mchg. Solomon Mwagisa toka ***Kanisa la Pentekoste Tanzania;*** Mchg. Grace Mbise toka ***Kanisa la Anglikana Tanzania;*** Bw. Brighton Killewa, ***Katibu Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania*** na Bibi Besetina Saikong, Mratibu wa ***Dawati la Utetezi*** KKKT.

## Programu ya Utawala Bora na Haki za Kijinsia

***Mradi wa Utawala Bora na Haki za Kijinsia*** ulianza 2014 hadi 2017. Eneo la Mradi ni Dayosisi Mashariki ya Ziwa Vicktoria, Dayosisi ya Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria na Dayosisi Mkoani Mara.

Programu inatekelezwa katika Kata zilizochaguliwa kwa kuzingatia mapendekezo ya upembuzi wa awali wa mradi uliofanywa katika maeneo yaliyo kithiri kwa vitendo vya ukatili. ***Kitengo cha Utetezi*** KKKT kinashirikiana na ***Kitengo cha Elimu*** KKKT katika mradi huu. Dayosisi husika zina shirikiana na Viongozi Serikali za Mitaa (Afisa Watendaji wa Vijiji, Kata, Madiwani na Halmashauri za Wilaya), Viongozi wa Mila pamoja na Viongozi wa Dini zote katika maeneo husika.

Mradi huu umeshafanyiwa tathmini na mafanikio yameonekana kwani ***Kamati za Utetezi*** zimeundwa na elimu ya ***utetezi, haki za binadamu na elimu ya sheria*** imetolewa. Kamati hizo zinafanya kazi vizuri katika maeneo ya mradi.

## WATOA MADA

**Bw. Jackson Muro toka CEDESOTA Mada yake ilihusu: "Dhana na Masuala ya Mabadiliko ya Tabianchi na Mazingira." [CEDESOTA: Community Economic Development and Social Transformation Network]. Aliyekaa ni Bw. Petro Ahham toka ANGONET mada yake ilihusu: "Wajibu wa Watendaji wa Serikali, Wananchi na Azaki katika Mipango, Sheria na Mikataba". [ANGONET: Arusha Non-Governmental Organization Network]. Mada kuhusu "Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Sekta za Uzalishaji na Huduma na Namna ya Kukabiliana Nayo" ilitolewa na Bw. Julius Norbert kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha (Mazingira).**



Viongozi mbalimbali wa dini na wawakilishi wa mashirika ya mazingira walishiriki 'Mdahalo wa Mabadiliko ya Tabianchi' uliofanyika Hoteli ya Corridor Springs, Arusha inayomilikiwa na Dayosisi ya Kaskazini Kati.

# Mkutano Mkuu ni Makumira tena


***NENO KUU: 'Jitahidi kuuhifadhi umoja wa roho katika kifungo cha amani,' (Efeso 4: 3)***

Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira kwa mara nyingine ni mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT). Tarehe za mkutano 12 - 14 Agosti 2015.

Neno Kuu: ***"Jitahidi kuuhifadhi umoja wa roho katika kifungo cha amani" (Efeso 4: 3).***

Mkutano Mkuu wa 18 ulifanyika Seminari Ndogo ya Kilutheri Morogoro 2011. Lengo ni kupokea, kujadili taarifa mbalimbali na kuweka malengo na mwelekeo wa miaka ijayo.

Mkutano Mkuu pia huchagua viongozi mbalimbali kama Mkuu wa KKKT, Mwandishi na Wajumbe wa Halmashauri, Bodi na Kamati mbalimbali za Kanisa.



**Askofu Mstaafu Prof. Hance Mwakabana.**

Mwongozaji wa Somo la Biblia ni Askofu Mstaafu Prof. Dkt. Hance Mwakabana. Na Somo hilo hutolewa tangu siku ya ufunguzi na kuendelea kwa siku zote za Mkutano.

## Mada za Mkutano Mkuu

**Zifuatazo ni Mada za warsha katika Mkutano Mkuu wa 19:**

- Umoja na Utambulisho Wetu katika Kuwajibika
- Umoja na Utambulisho Wetu katika Kuabudu
- Umoja na Utambulisho Wetu katika Neno na Sakramenti.




**Wajumbe katika Mkutano Mkuu wa 18 wa KKKT uliofanyika Seminari Ndogo ya Kilutheri Morogoro.**

# Dayosisi ya Kusini yatuma Wainjilisti kufanya ziara

Hivi karibuni KKKT Dayosisi ya Kusini ilituma Wainjilisti 23 na Wachungaji wawili kutoka Jimbo la Makambako kushiriki ziara ya mafunzo KKKT Dayosisi ya Kaskazini Kati na KKKT Dayosisi ya Meru.

Wageni hao walipofika Ofisi Kuu ya KKKT Arusha wakiongozwa na Mchg. Wallace Lupenza Mkuu wa Jimbo la Makambako walikutana na wajumbe wa menejimenti wakiongozwa na Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa.



**Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa, akiongea na ujumbe wa Wainjilisti toka Jimbo la Makambako, KKKT Dayosisi ya Kusini.**

# Mungaya kuongoza Idara ya Fedha na Utawala

Halmashauri Kuu ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) hivi karibuni ilimteua Bw. Loata Mungaya kuwa Naibu Katibu Mkuu Fedha na Utawala kushika nafasi ya Bw. Abel Mrema ambaye muda wake uliisha Desemba mwaka jana.

Kabla ya kujiunga na Ofisi Kuu ya KKKT iliyopo Arusha Januari mwaka huu, Bw. Mungaya aliwahi kuwa Mkaguzi Mwandamizi wa kampuni ya Pricewaterhouse Cooper ya Dar es Salaam 2001 - 2005; aliwahi kuwa Msaidizi wa Meneja wa Fedha wa Ker & Downey Safari ya jijini Arusha 2005 - 2009; Alikuwa Meneja wa Fedha wa Tanganyika Flying Company 2009 - 2011 na Mkaguzi wa Ndani wa Makampuni ya OMASI (Orkonerei Maasai Social Initiative) ya Arusha 2011 hadi Oktoba 2012.

Bw. Mungaya ambaye alizaliwa 30 Juni 1971 Kijiji cha Orkeeswa Wilayani Monduli ni mhitimu wa Shahada ya Uzamili katika Sayansi - Fedha na Vitega Uchumi ***(Master of Science - Finance and Investment)*** aliyoipata 2013 toka Chuo Kikuu cha Coventry cha London, Uingereza. Mwaka 2007 alitunukiwa Cheti cha CPA -PP-T kinachotolewa na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA). Alitunukiwa Shahada ya Biashara (Bachelor of Commerce) 2000 iliyotolewa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ameoana na Miriam na kwa pamoja wamebarikiwa kupata watoto watano.



**Bw. Loata Mungaya**
**Naibu Katibu Mkuu Fedha na Utawala, KKKT.**

# Mchg. Rohho ateuliwa kuongoza Misioni na Uinjilisti



**Mchg. Lazaro Rohho**
**Naibu Katibu Mkuu Mision na Uinjilisti, KKKT.**

Mchg. Lazaro Marcel Rohho amejiunga na Ofisi Kuu ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) kuwa Naibu Katibu Mkuu Misioni na Uinjilisti kuanzia Januari mwaka huu. Amechukua nafasi ya Mchg. Ambele Mwaipopo ambaye ameitikia wito kuwa Askofu wa Dayosisi ya Ziwa Tanganyika tangu mwezi Septemba mwaka jana.

Kabla ya nafasi hiyo mpya Mchg. Rohho alikuwa Mratibu wa Ofisi ya Huduma ya KKKT iliyopo Dar es Salaam kuanzia 2012 hadi 2014. Ana uzoefu wa muda mrefu baada ya kuwa Katibu Mkuu wa Dayosisi ya Mbulu kwa miaka saba (2005 - 2012).

Mchg. Rohho ambaye alizaliwa 21 Agosti 1965 Haydom Wilayani Mbulu, amehitimu Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira (TUMA) na kutunukiwa Shahada ya Masomo ya Dini (Bachelor of Divinity) 2000 na alitunukiwa Shahada ya Uzamili katika Theolojia (Master of Theology) mwaka 2003 hapo hapo Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.

Mwaka 2012 alihitimu Shahada ya Uzamili katika Biashara (Master of Business Administration) iliyotolewa na ESAMI (Eastern and Southern Africa Institute for Management) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha *Maastricht School of Management cha Uholanzi.*

Alibarikiwa kuwa Mchungaji 29 Aprili 2001 Usharika wa Haydom na kuhudumu nafasi tofauti katika sharika za Dayosisi ya Mbulu 2000 - 2005.

Ameoana na Grace na kwa pamoja wana watoto watatu - wavulana wawili na wa kike mmoja.

# Wachungaji Wanawake KKKT waadhimisha miaka 25



Wachungaji na Watheolojia wanawake KKKT walishiriki Kongamano mjini Bukoba Mei 2015.

Kongamano la Wachungaji na Watheolojia Wanawake wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) lilifanyika 12 - 17 Mei mwaka huu mjini Bukoba. Naibu Katibu Mkuu Huduma za Jamii na Kazi za Wanawake na Watoto, KKKT, Mchg. Rachel Axwesso, alisema hivi karibuni kwamba Kongamano hilo lilikuwa ni fursa ya kuadhimisha jubilii ya miaka 25 tangu Kanisa likubali kubarikiwa wanawake kuwa Wachungaji.

Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Alex Malasusa, alifungua kongamano hilo lililohudhuriwa na washiriki 170.

Wajumbe walimpongeza kwa kumpa zawadi Mchg. Alice Kabugumila toka Dayosisi ya Kaskazini Magharibi, ambaye ni mwanamke wa kwanza aliyesoma Mafunzo ya Theolojia KKKT. Alihitimu Stashahada katika Chuo cha Theolojia Makumira 1973. Alibarikiwa kuwa Mchungaji mwaka 2006. KKKT ina wachungaji na watheolojia wanawake 274.

# Vipindi vya dini vitumike ipaswavyo

**Na Timothy Franco Nkyandwale**

Kuanzia mwaka huu Dayosisi mpya ya Ziwa Tanganyika inatekeleza mpango wa ufundishaji wa vipindi vya dini katika Shule za Msingi ili kuijenga jamii yenye uelewa mpana na kulinda maadili ya kimwili na kiroho kwa wanafunzi.

Akiwa mjini Sumbawanga hivi karibuni Mkuu wa Jimbo la Rukwa, Mchg. Wilbrold Magwaya, alisema Kanisa lina nafasi kubwa ya kujengea watu uwezo wa kimwili na kiroho kwa kuanza na watoto wa shule.

Mchg. Magwaya alisema vipindi vya dini vilikuwa vikifundishwa vema miaka ya 1970 hadi ya 1980 katika Shule za Msingi na Sekondari. Baada ya hapo ufundishaji ulidorora.

Sababu za uhafifu ni ukosefu wa fedha, uhaba wa walimu wa kufundisha vipindi vya dini shuleni, ongezeko kubwa la shule na wanafunzi ikilinganishwa na miaka ya nyuma. Shule nyingi hazina walimu wa dini. Kutokana na tatizo hilo Dayosisi ikaweka mpango mahsusi ili kuhuisha Elimu ya Kikristo katika Shule za Msingi.

Hayo yamethibitishwa na Mratibu wa Elimu ya Kikristo wa Dayosisi, Mchungaji Alaika Kambo, aliyesema kuwa mipango imefanywa kama vile kuandaa miongozo na kuandaa walimu wa kufundisha somo hilo katika Shule za Msingi. Mchg. Kambo alifafanua kuwa Dayosisi imeandaa vifaa vya kufundishia, imetafiti kupata idadi ya wanafunzi na kuweka utaratibu wa kuwa na walimu wa kufundisha elimu ya dini shuleni, kwa kuzingatia muhtasari, nk.

Japo jukumu linapaswa kuwa la Mchungaji au Mwinjilisti lakini kwa kuwa idadi ya wanafunzi iliyopo ni kubwa sana kutokana na ongezeko la shule, inabidi mbinu mbadala zitumike kufanikisha kazi hiyo. Alitoa mfano kwamba katika Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga kuna shule za msingi 56 na zipo mbalimbali ambapo watumishi wa Kanisa ni wachache.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Chemchemi, Sumbawanga Mjini, Hancy Darnken, alikiri kuwa vipindi vya Elimu ya Kikristo havifundishwi, vipo kwenye ratiba kuu kama mapambo. Aliongeza kusema "baadhi ya madhehebu huleta mitihani ya mwisho kwa darasa la saba ili ifanywe mwishoni mwa mwaka, na sijui wanapima nini!" Alihoji.

Mkaguzi wa Shule za Msingi Sumbawanga ambaye hakutaka kutajwa jina lake, alisema vipindi vya dini havikaguliwi wafanyapo ukaguzi wa masomo mengine, ingawa huangaliwa kama vipo katika ratiba kuu ya shule au la. Alisema suala la dini ni la kiimani zaidi, hivyo viongozi wa dini husika inawapasa kutilia mkazo jambo hilo la sivyo mmomonyoko wa maadili utazidi. Alisema mafunzo ya dini ni nyenzo ya malezi ya kimwili na kiroho kwa jamii yenye kiu cha maadili.

Akiongea kwa njia ya simu, Afisa Taaluma Mkoa wa Mara, Atuvone Chaula, alisema kwa sasa jambo la kutofundishwa kwa somo la dini katika shule za msingi linaonekana kuwa ni hoja ya kawaida. Hivyo, viongozi husika inapasa kuweka mtaala wa masomo ya dini wazi kwa shule za msingi, kwani watoto ni nguzo ya taifa na vipindi hivyo vipo kisheria na elimu hiyo itakinusuru kizazi hiki kutoka katika dimbwi la utandawazi.

*Wasiliana na mwandishi 0754 651666*

# Askofu akemea wanasiasa wanaotumia vibaya Nyumba za Ibada



**Askofu Dkt. Frederick Shoo, KKKT Dayosisi ya Kaskazini.**

Askofu Dkt. Frederick Shoo wa KKKT Dayosisi ya Kaskazini amekemea tabia ya viongozi wa kisiasa kutumia nyumba za siasa vibaya. Alisema hivi karibuni kwamba "kanisani ni mahali pa ***Ibada Takatifu*** hivyo pasitumike kufanikisha ajenda za kisiasa."

Aliyasema hayo Mamba, Mkoani Kilimanjaro wakati wa Ibada ya kumbukumbu ya Marehemu Askofu Dkt. Stefano Moshi, aliyekuwa Askofu wa kwanza wa Dayosisi hiyo na Mkuu wa kwanza wa KKKT.

Dkt. Shoo ambaye ni Askofu wa wanne wa Dayosisi ya Kaskazini aliwekwa wakfu mwezi Januari katika Ibada iliyofanyika Usharika wa Moshi mjini kuchukua nafasi ya Askofu Dkt. Martin Shao aliyestaafu.



Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa, akigawa miche ya miti kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Loruvani, Arusha. Kanisa linahimiza utunzaji mazingira uende sambamba na upandaji miti ili kurejesha misitu inayotoweka haraka na kusababisha mabadiliko ya tabianchi.



Bw. William na Bibi Ester Kivuyo wakiwa na baadhi ya viongozi na watumishi wengine wa KKKT waliopanda miti na kushuhudia uzinduzi wa mtambo wa Biogesi katika kaya hiyo inayoishi Kijiji cha Kivulul, Arusha.

# Mjizatiti kutunza mazingira- wito

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) limetoa wito kwa Washarika wa KKKT na wana jamii kwa jumla kuhifadhi mazingira ili kutunza uhai na kupata maendeleo endelevu.

Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa, alisema hayo alipokuwa mgeni rasmi kuadhimisha Wiki ya Mazingira katika Kijiji cha Kivulul, Arusha. KKKT imeweka utaratibu wa kuadhimisha Wiki ya Mazingira juma la mwisho la mwezi Machi kila mwaka.

Walioshiriki ni wanakijiji, wanafunzi wa Shule ya Msingi Loruvani na watumishi wa Ofisi Kuu ya KKKT wakiwemo Bw. Mallumbo W.Mallumbo, Naibu Katibu Mkuu (NKM) Mipango na Maendeleo, Bw. Loata Mungaya, NKM Fedha na Utawala, Mchg. Lazaro Rohho, NKM Misioni na Uinjilisti na Mchg. Rachel Axwesso, NKM Huduma za Jamii na Kazi za Wanawake na Watoto.

Siku hiyo pia Katibu Mkuu alizindua mtambo wa biogesi katika kaya ya Bw. na Bibi Esther na Bw. William Kivuyo.

Kama inavyoonekana katika toleo hili la ***Uhuru na Amani,*** KKKT iko mstari wa mbele kutumia mbinu za kutunza **uumbaji wa Mungu** ikiwemo ya kuhamasisha jamii umuhimu wa kupanda miti**.**



Mratibu wa Kitengo cha Uhai na Mazingira KKKT, Patricia Mwaikenda pichani juu, aliyekuwa mwaandaji wa matukio Wiki ya Mazingira 2015, alisema biogesi ni nishati mbadala ambayo endapo itatumika na wengi itasaidia misitu isiteketee kwa ajili ya matumizi ya kuni na mkaa.



Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa, akizindua mtambo wa biogasi nyumbani kwa Bw. Wiliam na Bibi Ester Kivuyo wakati wa Wiki ya Mazingira 2015.

# Wainjilisti Dayosisi ya Konde ziarani



Naibu Katibu Mkuu Mipango na Maendeleo KKKT, Bw. Mallumbo Mallumbo, akizungumza na Wainjilisti 24 toka KKKT Dayosisi ya Konde waliofika Ofisi Kuu ya KKKT mwishoni mwa mwezi Oktoba kabla ya kuanza ziara ya KKKT Dayosisi ya Kaskazini Kati. Kiongozi wa msafara alikuwa ni Mchg. George Mwakanyamale ambaye ni Mkuu wa Jimbo la Kusini. Pia walitembelea Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.

# Hatimaye KKK-Congo kuna amani

Hatimaye mgogoro wa kiuongozi katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Congo (KKK-Congo) uliodumu zaidi ya miaka 12 umemalizika. Hatua hiyo imefikiwa baada ya pande mbili zilizokuwa zikisigana kukubaliana kuacha tofauti zao na badala yake kusonga mbele na kazi ya kueneza Injili na kufundisha Neno la Mungu jambo ambalo ndio msingi wa kuwepo kwa kanisa hilo.

Hatua hiyo chanya ilifikiwa katika Mkutano Mkuu wa Kanisa hilo uliofanyika katika Kituo cha Kilutheri cha Mafunzo ya Theologia Kimbeimbe, jijini Lubumbashi, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (DRC) 8 - 12 Aprili 2015.

Jumuiya ya Makanisa ya Kilutheri Eneo la Kati na Mashariki mwa Afrika (LUCCEA) ilikabidhi jukumu la usuluhisi kwa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT). Na mwaka 2012 timu ya usuluhishi ikiongozwa na Askofu Mstaafu Dkt. Erasto N. Kweka ilianza kuchukua hatua ya kuyaleta pamoja makundi mawili ndani ya Kanisa hilo yaliyokuwa yamefarakana.

Mpaka wakati muafaka ndani ya KKK-Congo unapatikana, Askofu Dkt. Kweka tayari alikuwa amewakutanisha meza moja viongozi wa makundi yaliyokuwa yamefarakana kwa muda mrefu ndani ya Kanisa hilo. Vile vile alipata nafasi ya kuonana na uongozi wa Serikali ya DRC Jimbo la Katanga jijini Lubumbashi ambao ulitoa ushirikiano mkubwa kusaidia kutatua mgogoro huo.

Askofu Ambele Mwaipopo Mkuu wa KKKT Dayosisi ya Ziwa Tanganyika, ambaye alikuwa mjumbe wa timu ya usuluhishi alisema hivi karibuni: "Maridhiano na muafaka uliotokea ni ***kazi ya Mungu anayeweza yote mahali pasipowezekana*** kwa kuitumia timu ya usuluhishi na wadau wengine wenye mapenzi mema na Kanisa la Mungu."



**Maaskofu wakati wa Ibada Takatikfu ya Meza ya Bwana baada ya Askofu Lunungu Tshambu na Askofu Kalumba Lusinge Bwino kuwekwa wakfu jijini Lubumbashi 12 Aprili 2015. Katikati mwenye joho jekundu ni Askofu Mstaafu Dkt. Erasto Kweka, Msuluhishi wa mgogoro wa KKK-Congo kwa niaba ya LUCCEA.**
**picha kwa hisani ya:** mchg. luke mwololo/ kelc


Kilele cha Mkutano Mkuu wa KKK-Congo kilikuwa 12 Aprili ambapo Ibada iliyojumuisha Wachungaji na Wakristo wa pande zote mbili ilifanyika. Ibada hiyo iliongozwa na Mkuu wa KKK-Congo, Askofu Mwamba Sumaili Rene. Katika Ibada hiyo, Askofu Lunungu Tshambu wa Dayosisi ya Congo West Kinshasa na Askofu Kalumba Lusinge Bwino wa Dayosisi ya Likasi waliwekwa wakfu.

Akihubiri katika Ibada hiyo na kujenga ujumbe wake katika Mdo. 2: 37 - 47, Askofu Kweka alifafanua mambo sita ambayo Wakristo wa kizazi hiki wanapaswa kuyashika kwa kuwa ndiyo msingi wa kukua na kuenea kwa Kanisa la kwanza.

Kwanza ni kule kudumu katika ushirika na Kristo; Kuhubiri na kufundisha Neno la Mungu; Kupenda Ibada na sala; Kuchukuliana mizigo; Kuwa na ushirika ambamo Mungu anatenda miujiza na maajabu na Ushirika wenye furaha na upendo.



**Askofu Ambele Mwaipopo,**
**KKKT Dayosisi ya Ziwa Tanganyika.**
**Askofu Mwaipopo aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Misioni ya KKK-Congo kwa miaka 13 (2001-2014).**



**Kushoto ni Askofu Kalumba Lusinge Bwino na Askofu Lunungu Tshambu waliowekwa wakfu 2015.**


Baadhi ya mapatano ya Mkutano Mkuu wa KKK-Congo ni pamoja na: Kuongeza Dayosisi zifike nane (kutoka tano zilizopo) zitakazoongozwa na Maaskofu na kuanzishwa kwa Dayosisi saba za maandalizi (za Misioni) zitakazoongozwa na Wachungaji. Hiyo KKK-Congo itakuwa na Dayosisi 15 miaka ijayo.

KKKT ni mwanzilishi wa Makanisa karibu yote ya Kilutheri katika nchi jirani, likiwemo KKK-Congo.


Soma **"Historia ya Kazi za Injili"** katika toleo hili la ***Uhuru na Amani.***

# Wapewa ridhaa kuendelea kuongoza

**Baadhi ya viongozi wa Dayosisi za Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) ambao vipindi vyao vya uongozi vilikuwa vimekwisha wameongezewa muda kama ifuatavyo:**



Mkutano Mkuu wa KKKT Dayosisi ya Kusini Magharibi umemchagua tena Askofu Job Mbwillo kwa kipindi cha miaka 4 kuanzia 2014. Askofu Mbwillo ameongoza Dayosisi hiyo tangu 1997.



Mkutano Mkuu wa KKKT Dayosisi Mkoani Mara umemchagua tena Askofu Michael Adam kwa kipindi cha miaka 4 kuanzia 2014. Askofu Adam ameongoza Dayosisi hiyo tangu 2009.

## Jukwaa la Wakristo Tanzania

Jukwaa la Wakristo Tanzania limetoa tamko la mkutano wa Maaskofu uliofanyika Dar es Salaam 10 Machi 2015 Wajumbe walitoka: Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC); Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) na Baraza la Makanisa ya Kipentekoste Tanzania (CPCT).

Kwa maelezo zaidi fungua tovuti:

**www.cct-tz.org/tamko-la-jukwaa/**

# Ushirika unajenga uchumi wa familia na jamii

**Na Elizabeth Lobulu**

***'Ushirika ni muhimu kujenga uchumi wa familia na jamii,'*** hayo yalisemwa na Mtendaji mkuu wa Chama cha SACCOS KKKT Dayosisi ya Kaskazini ambacho hadi sasa kina wanachama 2,000 tangu kianzishwe 1995. Hadi Novemba 2014 kimeweza kukopesha sh. Bilioni 6. Hivi karibuni kikundi cha watu 10 toka Ofisi Kuu ya KKKT iliyopo Arusha kilitembelea Ofisi ya SACCOS Dayosisi ya Kaskazini iliyopo Moshi ili kujifunza kutokana na mafanikio ya chama hicho.

Meneja na Katibu wa SACCOS ya KKKT Dayosisi ya Kaskazini, Bibi Monica Mlay, aliwapokea wageni hao akiwa katika ofisi mpya ya SACCOS hiyo. Na baada ya kuwapa historia fupi ya ofisi hiyo aliongoza mazungumzo na watumishi hao wa KKKT ambao ni viongozi na wajumbe wa Bodi ya SACCOS ya Ofisi Kuu ya KKKT.

Alisema ushirika wao ulianza kwa kusuasua lakini sasa wameweza kuwaajiri watumishi 4 wa kudumu kwa ajili ya kazi ya SACCOS akiwemo yeye mwenyewe ambaye ni mtumishi aliyeazimwa toka Dayosisi yake. Alisema uko umuhimu kwa uongozi wo wote wa SACCOS kuanza kwa kujifunza masuala ya ushirika na kuwa katika mtandao wa wadau wengine wa masuala ya ushirika. Alisisitiza umuhimu wa kuwaelimisha wanachama mara kwa mara kuhusu masuala ya ujasiriamali ili kwa pamoja SACCOS yao iweze kuwasaidia kuwa na maisha bora.



**Mwenyekiti wa SACCOs Ofisi Kuu ya KKKT, Bibi Florence Ngwijo, aliongoza wajumbe wa Bodi ya SACCOS kwa ziara ya mafunzo Dayosisi ya Kaskazini 31 Oktoba 2014. Picha ya pamoja ya watumishi hao na viongozi wa SACCOS Dayosisi ya Kaskazini.**

# Historia ya Kazi ya Injili KKKT

Mwaka 1887 kazi ya Injili kwa Kanisa la Kilutheri ilianzishwa nchini Tanganyika (baadaye Tanzania) na Chama cha "Misioni cha Berlin III" au "Evangelical Missionary Society for East Africa" (EMS) kutoka Ujerumani. Kituo cha kwanza cha misheni kilikuwa ni Kigamboni, Dar es Salaam.

Chama cha pili, yaani "Chama cha Misioni Berlin I", nacho kutoka Ujerumani, kiliingia Tanganyika kikitokea Afrika ya Kusini na kuanza kazi Nyanda za Juu Kusini mwaka 1891 kilipoanzisha kituo cha misheni sehemu iitwayo Ipagika au Pipagika (Wangemannshöhe) katika Dayosisi ya Konde.

Mwaka 1890 "Chama cha Berlin III" kilibadilika na kuchukua sura mpya baada ya kubadili sera yake na kujulikana kwa jina la "Bethel" au "Misioni ya Bethel". Misioni hii ikafika Tanga na kuanza kazi eneo la Mbuyukenda. Baadaye Misioni ya Bethel iliamua kufikisha Injili ya Kristo nje ya mipaka ya Tanganyika. Wamisioari waliohusika walipanga kwenda Rwanda kupitia Bukoba. Walipofika Bukoba mwaka 1910 wakashawishika kufungua kituo Bukoba na ile nia ya kuanzisha kazi ya misioni Rwanda ikawa imesitishwa.

Chama cha tatu kufika Tanganyika ni "Chama cha Misioni cha Leipzig" (nacho kilitokea Ujerumani). Kiliingia nchini mwaka 1893 na kuanza kazi ya misioni Kaskazini ya nchi kwa kuweka kituo cha misheni Kidia, Old Moshi.

Kutokana na vyama hivyo vitatu kijiti cha kueneza Injili kilipokelewa na wenyeji toka kwa wamisionari wa Ujerumani. Na vyama vingine vya misioni vilivyofika baadaye kutoka Ulaya na Marekani navyo vilieneza Injili kwa kufundisha Neno la Mungu kwa upendo na kwa usahihi, hasa baada ya Vita ya I ya Dunia (1914 - 1918) na Vita ya II ya Dunia (1939 - 1945).

Pamoja na kueneza Injili, Kanisa lilianza kutoa huduma mbalimbali za kijamii na diakonia kwa lengo la kumhudumia mwanadamu kikamilifu – kimwili, kiroho na kiakili.

Makanisa saba yanayojitegemea ambayo baadaye yaliungana na kuunda Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Tanganyika yalianzishwa. Na Juni 1963 Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanganyika (KKKT) likaundwa. Baada ya KKKT kuanzishwa Kanisa la Ubena-Konde (eneo la Nyanda za Juu Kusini) likaitwa Dayosisi ya Kusini; Kanisa la Uzaramo-Uluguru likaitwa Dayosisi Mashariki na Pwani; Kanisa la Usambara-Digo likaitwa Dayosisi ya Kaskazini Mashariki; Kanisa la Kaskazini likaitwa Dayosisi ya Kaskazini; Kanisa la Mbulu likaitwa Dayosisi ya Mbulu; Kanisa la Iramba-Turu likaitwa Dayosisi ya Kati na Kanisa la Kaskazini Magharibi likaitwa Dayosisi ya Kaskazini Magharibi.

Yapo maeneo nchini ambayo yalikuwa yanafanya kazi ya Injili kama misioni nayo ni: Mkoani Mara, Mashariki ya Ziwa Victoria, Ruvuma, Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Kusini Mashariki ambayo sasa ni Dayosisi.

Dayosisi za mwanzo nazo kwa kutegemea vigezo vya kikatiba na historia zikaendelea kugawanyika na hadi 2014 KKKT ikawa na Dayosisi 24 kama ifuatavyo: Dayosisi ya Kusini, Dayosisi ya Konde; Dayosisi ya Iringa; Dayosisi ya Kusini Kati; Dayosisi ya Kusini Magharibi; Dayosisi Mashariki na Pwani; Dayosisi ya Ulanga-Kilombero; Dayosisi ya Morogoro na Dayosisi ya Dodoma.

Nyingine ni Dayosisi ya Kaskazini Mashariki; Dayosisi ya Kaskazini; Dayosisi ya Kaskazini Kati; Dayosisi ya Pare; Dayosisi ya Meru; Dayosisi ya Mbulu, Dayosisi Mkoani Mara; Dayosisi ya Kati; Dayosisi ya Kaskazini Magharibi; Dayosisi ya Karagwe; Dayosisi Mashariki ya Ziwa Victoria; Dayosisi ya Ruvuma; Dayosisi ya Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria; Dayosisi ya Kusini Mashariki na Dayosisi ya Ziwa Tanganyika.

Pamoja na KKKT kuwa na Dayosisi 24 bado kuna maeneo machache nchini ambayo ni ya misioni. Maeneo ya Misioni ndani ya nchi ni: Zanzibar, Kigoma na Tabora.

Pia KKKT inafanya kazi ya misioni nchi jirani kwa kushirikiana kwa hali na mali na makanisa dada na mashirika ya misioni toka ng'ambo. Katika misioni hizo watumishi hutumwa kuanzisha kazi ya misioni lakini pia washarika wa KKKT wamekuwa chachu ya kuanzishwa misioni nchi jirani.

Juhudi za kazi ya misioni ya nje zimesaidia kuzaa makanisa katika nchi jirani ambayo yanalelewa na KKKT. Misioni ya KKKT nje ya nchi ni katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya watu wa Kongo (DRC), Kenya, Zambia, Msumbiji, Rwanda, Burundi na Uganda.

Yafuatayo ni maelezo mafupi ya Misioni ya KKKT nchi jirani. Wamisionari wa KKKT walitumwa kwenda Kenya miaka ya 60 (wakati wa Jumuiya ya Afrika Mashariki) baada ya kupokea ombi la Walutheri toka Tanzania waliokuwa Nairobi na Mombasa kuomba huduma ya kiroho toka KKKT. Baada ya KKKT kuanza huduma hiyo moja ya makanisa mawili ya Kilutheri Kenya ilikuwa ni Sinodi ya KKKT iliyojulikana kama "KKKT Sinodi ya Kenya". Wajumbe wawili walikuwa wakihudhuria vikao vya Halmashauri Kuu ya KKKT kwa muda mrefu hadi walipounda Kanisa lao linalojitegemea.

Viongozi wa Kanisa la Kongo walisafiri toka Lubumbashi hadi Nairobi wakiulizia iliko "Redio Sauti ya Injili" ambayo ilikuwa na studio zake Moshi. Huko Kenya wakadhani iko Dar es Salaam. Walipofika Dar es Salaam wakaelekezwa studio iko Moshi na walipofika huko walikutana na viongozi wa KKKT. Ombi la Viongozi hao wa Kongo lilikuwa kujiunga na Kanisa hilo ambalo habari zake wamezisikia kupitia masafa mafupi ya "Redio Sauti ya Injili". Na huo ndio uliokuwa mwanzo wa misioni na baadaye kuanzishwa kwa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Congo (KKK-Congo).

Nalo Shirika la Kikristo la Huduma kwa Wakimbizi (TCRS) kwenye miaka ya 70 liliomba KKKT itoe huduma za kiroho kwa wakimbizi. Na kutokana na kazi hiyo, wakimbizi waliporudi kwao waliweza kuandeleza kazi ya misioni na hatimaye makanisa ya Kilutheri nchini Msumbiji, Rwanda na Burundi yalianzishwa.

Katika kazi hiyo ya misioni ya nje ya nchi, KKKT inatoa fursa ya masomo ya theolojia kwa watumishi wazawa ili kusaidia kuenea kwa Injili ya Kristo kwa kasi zaidi katika nchini husika.

**Wakala**

**Gazeti la Uhuru na Amani**

Unapolipa kwa TT NBC; tafadhali tuma kivuli cha Pay-in-Slip kwa Mhariri kwa njia ya Barua Pepe: <elobulu@elct.or.tz>

A/C ni ile ile: Na: 014103002064

# Upendo FM 107.7



*Amani kwa wote*

**JE UNAFAHAMU KITUO BORA CHA REDIO KATIKATI YA JIJI?**

Kwa matangazo ya biashara na mikutano ya Injili, kwa ushauri wa kiroho na maendeleo ya jamii: Tangaza kwenye Redio bora ya Upendo na Amani kwa wote.

Fika sasa LUTHER HOUSE
GHOROFA YA PILI
SOKOINE DRIVE.

Upendo FM 107.7 Mhz
P.O. Box 13603
Da es Salaam, Tanzania

Simu: 022 212 4228/ 2139556/ 2124221
E-mail: upendofm@yahoo.com

# Radio Utume Lushoto

**KKKT DAYOSISI YA KASKAZINI MASHARIKI YENYE MAKAO YAKE MAKUU MJINI LUSHOTO, MKOA WA TANGA, ITAZINDUA KITUO CHA REDIO UTUME KATIKA MASAFA YA FM HIVI KARIBUNI.**

# Radio Furaha 96.7 FM

Sikiliza matangazo ya kituo bora cha Redio Iringa na maeneo jirani.

Kwa maoni, ushauri wa kiroho na kijamii wasiliana na:

Meneja: Protas Kanemela
Simu: +26 27 003 43

Fax: +255 262 701 198
Barua pepe: elctrd1987@yahoo.com

# Ifahamu

## RADIO SAUTI YA INJILI

FM 92.2 & 96.2 MHz
MOSHI

**RSYI ni rafiki anayekujali kiroho na kimwili.**

Katika Masafa ya FM, Radio Sauti ya Injili kutoka Moshi inasikika vizuri kabisa katika Masafa yafuatayo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Moshi | 92.2 MHz | Mlalo (Lushoto) | 102.6 MHz |
| Arusha | 96.2 MHz | Kisosora (Tanga) | 96.7 MHz |
| Same | 100.4 MHz | Morogoro | 96.6 MHz |
| Kibaya (Kiteto) | 102.9 MHz | Hakwe (Rombo) | 96.4 MHz |

**Aidha Radio Sauti ya Injili, Moshi inasikika kwenye tovuti dunia nzima kwa saa 24 www.sautiyainjili.org**

Radio Sauti ya Injili inatangaza vipindi mbalimbali vikiwemo vya maendeleo, afya, uchumi, habari na halikadhalika vipindi vya mafundisho ya dini. Unaweza kupata habari moto moto za kitaifa na kimataifa katika kipindi cha Dira ya Leo.

Wasiliana na:
Mkurugenzi RSYI
S.L.P. 777, Moshi

Simu: 027 27 52772 au 027 27 53080
E-mail: redio@elct.org
Tovuti: www.sautiyainjili.org

**Kumbuka kuwa RSYI ipo kwa ajili yako. Aidha, kijamii. Endelea kuimarisha huduma nzuri hii kwa hali na mali.**